NORTH EASTERN DIOCESE

EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA
P. O BOX 10 (TEL 027-2640027 FAX 027-2660092) LUSHOTO

BUMBULI CLINICAL OFFICER'S TRAINING CENTER

JINA LA MWANAFUNZI: ……

YAH: MAFUNZO KWA MWAKA WA MASOMO 2019/2020
DIPLOMA CLINICAL MEDICINE

Napenda kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya Diploma Clinical Medicine katika chuo hiki cha Bumbuli.

Mafunzo haya ni ya mwaka mmoja (1) kwa Diploma (Upgrading) na miaka **3** kwa Diploma Clinical Medicine Direct entry unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe **07.10.2019**. Tarehe ya mwisho ya kupokelewa chuoni ni tarehe **15.10.2019.**

Gharama ya mafunzo ni **Sh. 2,005,000.00** (shilingi million mbili na elfu tano tu) kwa mwaka. Unaweza kulipa ada hii kwa awamu moja, mbili au tatu. Malipo yote ya Ada yanapaswa kufanywa benki kwa kupitia akaunti ifuatayo: **NMB ELCT NED CLINICAL OFFICERS TRAINING CENTRE: A/C NO. 41601300005**.

Utaratibu wa malipo ni kama ifuatavyo:

A: Fedha zifuatazo zilipwe kabla ya mwanafunzi kufika chuoni.

- Mwanafunzi anatakiwa alipe shilingi **844,800/=** kwenye akaunti (NMB Lushoto,ELCT NED CLINICAL OFFICERS TRAINING CENTRE A/C No.4161300005).
- Ada kwa ajili ya mtihani wa NACTE **shilingi 150,000/=** Unatakiwa kulipia katika akaunti ya mitihani ya taifa ambayo ni (A/C No. 20110007946 Application and Examination fee Account) malipo haya hayapo ndani ya ada.

- Ada kwa ajili ya shughuli za wanafunzi ya shilingi elfu **18,000/=** (SEKOMU –SO A/C No 43410000048 NMB).
- Mwamafunzi asiye na Bima ya afya anatakiwa kulipia Kiasi cha Tsh 50,400/- katika account ya chuo (**NMB ELCT NED CLINICAL OFFICERS TRAINING CENTRE: A/C NO. 41601300005)**.

B: Kiasi cha shilingi 572,200/= kitalipwa tarehe 28.02.2020.

C: Kiasi kilichobaki cha Sh. 564,800/= kitalipwa mwanzoni mwa muhula wa pili.
Kabla ya kuripoti chuoni, hakikisha afya yako imepimwa na dakitari kwenye Hospitali au kituo cha Afya kinachotambuliwa na serikali. Mara ufikapo chuoni, utatakiwa kumkabidhi mkuu wa chuo cheti (Medical Certificate) kutoka kwa daktari aliyekupima.

Wakati wote uwapo chuoni, utatakiwa kutii sheria za nchi na za Chuo. Masuala yote ya wanafunzi chuoni yatashughulikiwa na Uongozi wa Chuo. Endapo patakuwa na haja ya suala la mwanafunzi kushughulikiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (Makao Makuu), jambo hilolitatakiwa kuwasilishwa kwanza kwa Mkuu wa Chuo kabla ya kupelekwa Wizarani. Gharama zote za usafiri wa kwenda na kurudi chuoni ni jukumu la mwanafunzi kwa kipindi chote atakapokuwa chuoni. Hakikisha unakuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi binafsi kwa kipindi chote utakachokuwa chuoni.

UNATAKIWA KUFIKA CHUONI NA VIFAA VIFUATAVYO

1. **SARE ZA CHUO**

   (MWAFUNZI WAKIKE)

- Magauni mawili (2) meupe ya mikono mifupi na urefu chini ya magoti usiopungua sentimita kumi (10cm).
- Viatu vyeupe, vyeusi au kahawia vyenye visigino vifupi.
- Makoti mawili meupe ya mikono mirefu, yawe marefu chini ya magoti urefu usiopungua sentimita kumi (10cm).

(MWANAFUNZI WA KIUME)

- Suruali mbili (2) za rangi ya kaki.
- Mashati mawili rangi nyeupe ya mikono mifupi.
- Viatu vya ngozi nyeusi au kahawia.
- Makoti mawili meupe ya mikono mirefu, yawe marefu chini ya magoti urefu
- usiopunguia sentimita kumi (10cm).

ANGALIZO:

- Ni muhimu kuhakikisha kwamba mavazi yanatunza heshima yako naya chuo, hivyo mavazi yasibane wala kuangaza kwa namna inavyoonesha maumbile ya mwili. Hata hivyo mwanafunzi anatakiwa kuvaa nguo za heshima wakati wote atakapokuwa chuoni.
- Kutakuwa na masweta kama sale ya chuo, yatapatikana chuoni kwa bei elekezi ambayo itapangwa na chuo, hii ni kwa wote wavulana na wasichana.

2. MAHITAJI YA USAILI, WODINI NA BWENINI

- Picha nne passport size kwa ajili ya kumbukumbu.
- Cheti halisi (original) cha kuhitimu kidato cha nne.
- Vitabu katika kozi husika inapowezekana.
- Vifaa vya kuandikia mfano kalamu,rula,madaftari n.k
- Mwamvuli au koti la mvua na buti za mvua.
- Shuka 4,Mto 1,Blanket 1,chandarua 1 taulo na foronya.
- Blood pressure machine.
- Stethoscope.
- Clinical torch.
- Tape measure.
- Thermometer.
- Patella hammer.
- Turning fork.
- Stop watch.
- Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na “Rim paper” moja (1)
- **Unashauriwa pia kuja na laptop ili kurahisisha mafunzo**

AINISHO LA ADA NA GHARAMA NYINGINE:
S/N ITEM COST

S/N	ITEM	COST
1	Tuition Fees	**1,340,000.00/=**
2	Identify card	**12,000.00/=**
3	Caution money	**10,000.00/=**
4	Internal examination costs and practical activities	**230,000.00/=**
5	NACTE student registration fee	**15,000.00/=**
6	Computer facilities & Services	**60,000.00/=**
7	Student Activities fee (to be paid to Bumbuli Campus SEKOMU- SO A/C No. 43410000048)	**18,000.00/=**
8	Quality Assurance fee	**20,000.00/=**
9	Special Faculty Requirements fee	**300,000.00/=**
	Total Amount	**2,005,000.00/=**

MALAZI

- Chuo kwa sasa hakina hostel za kutosha kuchukua wanafunzi wote. Kipaumbele kitatolewa kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza, wanafunzi wa kike, wenye mahitaji maalum na wageni.
- Gharama ya Kuishi ndani ya hostel za Chuo kwa muhula ni **Sh. 200,000** (shilingi laki mbili tu) na kwa mwaka wote wa masomo ni **Sh. 400,000** (shilingi laki nne tu).
- Fedha hizo zaweza kulipwa kwa mara moja au awamu mbili kupitia akaunti ya Chuo (NMB Lushoto, ELCT NED CLINICAL OFFICERS TRAINING CENTRE A/C NO.4161300005).
- Wanafunzi watakaokosa nafasi kwenye hostel za Chuo watapangiwa kwenye hostel za watu binafsi zilizohakikiwa na Chuo na kukidhi vigezo. Kwa mawasiliano kuhusiana na hostel za nje ya Chuo wasiliana na 0787181682/0712268602.

CHAKULA

- Chakula kwa kipindi chote cha mafunzo ni gharama ya mwanafunzi.
- Chakula hupatikana maeneo ya Chuo kwa fedha taslim.

MAELEKEZO KUHUSU MAHALI CHUO KILIPO

- Chuo kipo Bumbuli katika halmashauri ya Bumbuli, Wilaya ya Lushoto mkoa wa Tanga.
- Ukitokea upande wa kaskazini kama Arusha, Moshi n.k au upande wa mashariki kama Dar es salaam panda basi liendalo moja kwa moja Bumbuli.
- Endapo hutapata basi liendalo moja kwa moja Bumbuli, waweza kupanda basi lolote hadi Mombo kisha basi jingine hadi Soni kisha upande mabasi yaendayo Bumbuli.

KARIBU SANA BUMBULI

.....

MKUU WA CHUO – BUMBULI COTC